

**HOTUBA YA RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA
MAPINDUZI MHESHIMIWA DK. HUSSEIN ALI MWINYI KATIKA
UZINDUZI WA MAADHIMISHO YA WIKI YA SHERIA, DODOMA**

TAREHE: 23 JANUARI, 2022

**Mheshimiwa Prof. Ibrahim Hamis Juma;
Jaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania;**

**Mheshimiwa Dr. Tulia Ackson
Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungao**

**Mheshimiwa George Boniface Simbachawene (Mb);
Waziri wa Katiba na Sheria,**

**Mheshimiwa Khamis Ramadhan Abdalla;
Kaimu Jaji Mkuu wa Zanzibar,**

**Mheshimiwa Antony Mtaka;
Mkuu wa Mkoa wa Dodoma,**

Waheshimiwa Majaji wa Mahakama ya Rufani,

Mheshimiwa Mustapher Mohamed Siyani; Jaji Kiongozi,

Waheshimiwa Majaji wa Mahakama Kuu,

**Prof. Elisante Ole Gabriel Laizer;
Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania,**

**Mheshimiwa Wilbert Chuma;
Msajili Mkuu Mahakama ya Tanzania**

Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama,

Wasajili, Wakurugenzi na Watendaji wa Mahakama,

Mahakimu na Mawakili,

Viongozi wa Vyama vya Siasa,

Viongozi wa Dini,

Waandishi wa Habari,

Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana.

Kwanza kabisa, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu; mwingi wa rehema kwa kutujalia uhai na afya njema na kutuwezesha kuufikia mwaka mpya 2022 tukiwa salama. Kadhalika, napenda kuwapongeza Watanzania wote kwa kufanikisha Maadhimisho ya miaka 60 ya uhuru wa Tanzania Bara na miaka 58 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar kwa mafanikio makubwa ya umoja, amani na mshikamano. Hii ndiyo misingi mikubwa na muhimu ya maendeleo ambayo Watanzania wanaendelea kuyashuhudia katika sekta zote nchini ikiwemo muhimili wa Mahakama na vyombo vyengine vya sheria na utawala bora.

Natoa shukurani zangu za dhati kwako; Mheshimiwa Jaji Mkuu wa Tanzania; Profesa Ibrahim Hamis Juma kwa kunialika kuwa Mgeni Rasmi

katika hafla hii ya uzinduzi wa maadhimisho ya wiki ya sheria kwa mwaka huu wa 2022.

Mheshimiwa Jaji Mkuu na Wageni Waalikwa,

Nimejulishwa kwamba, tokea mwaka 1996, Mahakama ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imejiwekea utamaduni wa kuadhimisha Siku ya Sheria ikiwa ni kuashiria kuanza kwa mwaka mpya wa Mahakama. Aidha, nafahamu kuwa, Siku ya Sheria hutanguliwa na Wiki ya Sheria ambayo kwa mwaka huu 2022, Mahakama ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imenipa heshima mimi kuja kuizindua Wiki hiyo, leo hii tarehe 23 Januari, 2022. Nakushukuruni sana.

Mheshimiwa Jaji Mkuu na Wageni Waalikwa,

Katika wadhifa wangu wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na mtu niliyeitumikia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa nafasi za uwaziri, natambua na kuheshimu sana, nafasi na umuhimu wa Sheria kwa pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nafahamu kwamba sheria ina umuhimu mkubwa katika kujenga umoja wetu, amani yetu, udugu wetu, na pia mshikamano wetu. Mafanikio ya kiuchumi, kibiashara na kiuwekezaji, hutegemea kuwepo kwa misingi ya utawala wa sheria na uhuru wa Mahakama. Ni dhahiri kuwa ustawi wa wananchi wetu, pamoja na mambo mengine kwa kiasi kikubwa yatategemea kuwepo kwa sheria madhubuti inayotambua ukweli kuwa, wananchi wetu wa pande zote mbili za Muungano, wengi wao ni masikini.

Kwa hivyo, wanatarajia kuwa sheria zetu na taratibu za Kimahakama zinasaidia kuwainua na kufanikisha shughuli zao za kiuchumi na kijamii. Kuwepo kwa sheria bora zinazosimamiwa vyema, ndiko kutafanikisha uchumi wao, biashara zao na shughuli zao za kila siku za kujitafutia kipato.

Mheshimiwa Jaji Mkuu na Wageni Waalikwa,

Kwa upande wa Zanzibar kwa mfano, dhamira ya Serikali ya kujenga uchumi wa kisasa unaozingatia matumizi sahihi ya rasilimali za bahari au kama unavyofahamika Uchumi wa Buluu, ni jitihada za dhati kabisa za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kujenga uchumi utakaowasaidia wananchi wa Zanzibar. Vile vile, kwa upande wa pili wa Tanzania, kuna dhamira ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kupunguza umaskini na kuwa na uchumi unaolingana na ushindani wa Karne ya 21. Ni dhahiri kuwa kufanikiwa kwa dhamira na jitihada hizi za Serikali zetu zote mbili, kutategemea uwezeshi na mchango mkubwa wa sekta ya sheria na hasa kupata ushauri wa kitaalamu kutoka kwa wanasheria wetu.

Kwa hivyo, natumia fursa hii adhimu ya uzinduzi wa maadhimisho ya wiki ya sheria, kutoa wito kwa Wanasheria na wataalamu wote wa sheria, kwa viongozi wa Mahakama na watumishi wote wa sekta za sheria kuielewa na kuifanyia kazi mipango yetu mikuu ya uchumi na kuwa huru kutoa ushauri wenu wa kisheria Serikalini kwa lengo la kuifanikisha. Tunatambua kuwa zipo sheria ambazo huenda zikawa ni kikwazo cha kufikia matarajio yetu ya kiuchumi na ustawi wa jamii. Sheria hizo zitahitaji kufanyiwa mabadiliko ili

zifanikishe mipango yetu ya uchumi wa kisasa. Kwa hivyo, tumieni utaalamu wenu kuzishauri Serikali zetu kuchukua hatua za kurekebisha sheria ambazo zina kasoro nasi tutafanya hivyo kwa maslahi mapana ya nchi yetu na Watanzania wote.

Mheshimiwa Jaji Mkuu na Wageni Waalikwa,

Katika hotuba yangu ya tarehe 11 Novemba, 2020, nilipokuwa nikilizindua Baraza la Kumi la Wawakilishi Zanzibar, niliweka wazi dhamira yangu ya kuijenga Zanzibar mpya, yenye uchumi wa kisasa wa Buluu (Blue Economy). Uchumi wa Buluu ni matumizi endelevu ya rasilimali za bahari. Huu ni uchumi unaofungamanisha kwa pamoja sekta za uvuvi, ufugaji samaki, ujenzi wa viwanda vya kusindika samaki, ukulima wa mwani, uchimbaji wa mafuta na gesi, pamoja na shughuli za utalii wa fukwe na michezo ya baharini. Katika hotuba yangu hiyo, niliwakumbusha Wawakilishi kwamba Zanzibar ina haja ya kufanya mabadiliko ya kiuchumi kwa kuzitumia ipasavyo rasilimali za bahari kutokana na kuwepo kwa udogo wa ardhi huku idadi ya watu wake ikiendelea kuongezeka. Katika hotuba hiyo nilisema, ninanukuu:

"Zanzibar hatukujaaliwa ardhi kubwa. Nchi yetu ni visiwa. Idadi ya watu wetu imeongezeka mara tano katika kipindi cha miaka 56. Mwaka 1964 Wazanzibari tulikuwa laki 3 tu, leo tuko takribani milioni 1.6. Wakati huo huo Visiwa vyetu havipanuki wala kuongezeka. Ndio kusema, ardhi yetu inazidi kuwa finyu mwaka hadi mwaka. Ahueni tuliyonayo ni

kuwa na eneo kubwa la bahari. Hivyo sisi Wazanzibari hatuna budi tuigeuze bahari hii kuwa ndio shamba letu. Huko ndiko fursa na ajira za Zanzibar mpya zilipo. Huu ndio msingi wa dhana nzima ya Uchumi wa Buluu.”

Mheshimiwa Jaji Mkuu na Wageni Waalikwa,

Ni matumaini yangu kuwa, tukielewa dhana ya uchumi wa Buluu, tutakuwa katika nafasi nzuri ya kurekebisha na kuboresha sheria na taratibu za Mahakama, na kuondoa vikwazo au vizingiti vyote katika safari yetu tulioidhamiria ya kujenga uchumi wa Buluu kwa upande wa Zanzibar. Kwa lugha nyingine, sheria na taratibu za Mahakama zilizopo lazima ziendane na mipango iliyopo ya Serikali yenye lengo la kuboresha maisha ya wananchi kupitia Uchumi wa Buluu. Mimi binafsi nitafurahi sana kama wanasheria kutoka pande zote mbili za Muungano, mtakuwa na mijadala ya dhati kuhusu kwa kiasi gani, sheria na taratibu za kimahakama zinavyoweza kuboreshwa kwa lengo ya kufanikisha dhamira ya Serikali ya Mapinduzi Awamu ya Nane ya ujenzi wa uchumi wa buluu.

Mheshimiwa Jaji Mkuu na Wageni Waalikwa,

Napenda nitumie fursa hii ya uzinduzi wa maadhimisho ya Wiki na Siku ya Sheria, kukumbusha umuhimu wa kuzingatia maadili katika utoaji haki. Katika hotuba zangu tangu nichaguliwe kuwa Rais wa Zanzibar, nimekuwa nikisisitiza umuhimu wa kuheshimu sheria kwa vile natambua kuwa miongoni mwa mambo yanayodhoofisha misingi ya utawala bora ni kuwepo

kwa vitendo vya rushwa, ubadhirifu, uzembe, kukosa uwajibikaji, na kutofuata sheria na kukiukwa kwa maadili.

Nachukua fursa hii kupongeza jitihada mbali mbali zinazochukuliwa na Mahakama ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuimarisha huduma za kutoa haki kwa wananchi na kuhakikisha mnaongeza kasi ya kusikiliza mashauri mbali mbali yanayowasilishwa katika ngazi zote za Mahakama. Napongeza sana hatua ya kuanzisha mahakama inayotembea kwani imesadia sana kuweza kuwafikia wananchi wa maeneo mbali mbali na kunufaika na huduma hiyo. Kadhalika, napongeza hatua zilizoanza kuchukuliwa za kutafsiri sheria zetu kwa lugha ya Kiswahili jambo ambalo limewapa matumaini na kufurahiwa na Watanzania kama hatua mojawapo ya maendeleo ya sekta ya sheria nchini. Ni vyema sasa tuongeze jitihada za kupata wataalamu wa lugha ya alama pamoja na kuimarisha miundombinu inayozingatia uwepo wa Watanzania wenye mahitaji maalum wakiwemo watu wenye ulemavu wa aina tofauti.

Binafsi, nimeridhishwa sana na hatua ya ushirikiano iliyopo baina ya Mahakama ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mahakama ya Zanzibar. Imeelezwa kuwa uhusiano huo ni wa muda mrefu tokea mwaka 1965. Nafurahi kuona kuwa ushirikiano huo unaendelezwa kwa kupeana uzoefu na utaalamu utakaoongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yenu. Natoa wito kuuendeleza ushirikiano huo kwa lengo la kuwa chachu

ya kuleta mabadiliko ya utendaji na kuongeza kasi ya ufasini katika mahakama zetu.

Mheshimiwa Jaji Mkuu na Wageni Waalikwa,

Napongeza mafanikio makubwa niliyoyaona wakati nikitembelea maonesho yaliyoandaliwa. Nimeelezwa kuwa huduma zinazotolewa katika juma lote la maadhimisho, ni moja ya utekelezaji wa nguzo ya tatu ya Mpango Mkakati wa Mahakama. Malengo makuu ya nguzo hiyo ni pamoja na kuimarisha imani ya Wananchi, kwa kuongeza uelewa na ufahamu wao wa taratibu na shughuli za utoaji haki nchini. Nakubaliana na uwamuzi wa kuzidi kutoa taaluma kuhusu huduma za Mahakama kwani bado taaluma hii haijaweza kuwafikia wananchi walio wengi. Ni wazi kuwa wananchi wetu wataonufaika sana na huduma hii na nitowe wito kwao kuja kwa wingi na kuitumia vizuri.

Nakiri kwamba maandalizi ya maonesho niliyoyaona kuanzia mpangilio wa mabanda yenyewe, huduma zinazooneshwa, elimu inayotolewa na weledi wa watoa elimu hiyo ni ishara nzuri kuwa kazi kubwa ya matayarisho imefanyika. Hongereni sana. Kupitia maonesho haya, pia nimeshuhudia maboresho makubwa yaliyofanywa na yanayoendelea kufanywa katika mnyororo mzima wa utoaji haki. Ni dhahiri kuwa maboresho makubwa niliyoshuhudia ya matumizi ya TEHAMA ni dalili njema ya matayarisho makubwa ya kupokea na kuendeleza matumizi ya Tehama ndani ya Mahakama.

Natoa pongezi za kipekee kwa uongozi wa Mahakama ya Tanzania na watumishi wote wa Mahakama kwa kuendeleza maboresho haya makubwa. Natoa rai kwa uongozi wa Mahakama ya Tanzania kuwa karibu na uongozi wa Mahakama za Zanzibar katika kusaidia maboresho kama haya yaweze pia kufanyika Zanzibar, ili kuongeza ufanisi wa shughuli za mahakama zetu.

Natoa wito kwa wananchi wote wa Mkoa wa Dodoma na Mikoa ya jirani kuitumia fursa hii kwa kufika kwenye mabanda haya na kupata huduma zinazotolewa bila ya malipo.

Mheshimiwa Jaji Mkuu na Wageni Waalikwa,

Napenda niupongeze pia uongozi wa Mahakama kwa kupanga matembezi ya leo kabla ya shughuli za uzinduzi wa Wiki ya Sheria. Sote tunafahamu umuhimu wa kufanya mazoezi kila siku kwa madhumuni ya kulinda afya zetu. Nimefurahi sana kuona kwamba wote tulioanza nao matembezi wakiwemo wazee wetu Waheshimiwa Majaji wa Mahakama ya Rufani na wewe Mheshimiwa Jaji Mkuu tumemaliza matembezi tena kwa mwendo tulioanza nao. Hakika hii ni ishara kuwa Mahakama na Wadau wake sio wabobezi tu katika tasnia ya sheria, bali pia mnafahamu umuhimu wa kufanya mazoezi ya viungo ili kuzifanya afya zenu ziwe imara.

Mheshimiwa Jaji Mkuu na Wageni Waalikwa,

Nimefarijika kuona kuwa Wiki ya Sheria itatumika pia kutoa huduma ya chanjo ya kujikinga na UVIKO 19. Nami niungane na Mheshimiwa Jaji Mkuu

kwa kuwahimiza watumishi wote wa Mahakama na wananchi ambao bado hawajachanja kufika katika maeneo haya ya maonesho ili kupata chanjo ambayo itatolewa na wataalamu wetu wa afya.

Mheshimiwa Jaji Mkuu, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;

Baada ya maelezo haya sasa natamka kuwa Wiki ya Maadhimisho ya Siku ya Sheria Nchini kwa mwaka 2022 imezinduliwa rasmi.

MUNGU IBARIKI TANZANIA.

MUNGU IBARIKI MAHAKAMA YA TANZANIA.

Asanteni kwa Kunisikiliza